

## maambukizi ya SARS-CoV-2




## chanjo za UVIKO-19 zinazotumika nchini Uingereza

### Inama anisha nini kwako



- Unaweza kudhoofika na UVIKO-19.
- Uwezekano wa kuendeleza magonjwa ya muda mrefu (UVIKO 19 wa muda ndefu).
- unaweza kueneza virusi kwa wengine.



- Hupunguza kwa kiasi kikubwa uwezekano wa kupata UVIKO-19, kuwa mgonjwa na kifo.
- Huleta mwitikio wa kinga katika njia **salama na iliyodhibitiwa**.
- Hupunguza uwezekano wa kueneza virusi kwa wengine na kupata UVIKO kwa muda mrefu.
- Haiwezi kukusababishia UVIKO-19.

### Mwitikio wa kinga




- **Inatofautiana kwa kiasi kikubwa** kati ya watu. Sababu nyingi huathiri ufanisi wa mwitikio wa kinga mfano, umri.
- Inaweza kuhusishwa na madhara ya ugonjwa; watu wanaopata ugonjwa wana uwezekano mkubwa wa kuwa na viwango vya juu vya kingamwili.




- Hutofautiana lakini wengi (hata wazee) huzalisha **mwitikio wenye nguvu wa kinga**.
- Dozi ya chanjo ya nyongeza inaboresha kinga.
- Chanjo huongeza kinga ambayo ipo kutokana na maambukizi ya awali.

### Muda wa kinga




- Haijulikani kikamilifu; ulinzi hupungua kadiri ya muda, na muda hutofautiana kati ya watu.
- Watu wengi huhifadhi seli za kinga ambazo **hutoa ulinzi dhidi ya magonjwa**.




- Utafiti unaendelea, lakini hadi sasa dozi mbili hutumika **kulinda dhidi ya magonjwa** ingawa ulinzi hupungua kadiri ya muda, na muda hutofautiana kati ya watu.
- Dozi ya nyongeza inaboresha muda wa kinga.

### Aina za chanjo



- **Maambukizi mapya kawaida husababishwa na aina ya Omicron.**
- Utafiti unaendelea kuhusu athari za virusi kwenye kinga dhidi ya maambukizi ya awali.
- Kingamwili zinaweza kuwa na ufanisi mdogo dhidi ya maambukizi mapya na aina tofauti za virusi, wakati seli za T zinaweza kutoa kinga zaidi.



- **Dozi tatu hutoa ulinzi wakutosha** dhidi ya aina nyingi ya virusi vya sasa.
- Utafiti unaendelea kuhusu athari za virusi kwenye kinga dhidi ya chanjo
- Maambukizi yanaweza kutokea lakini baada ya chanjo ya nyongeza kuna uwezekano wa kusababisha dalili nyepesi na za kawaida.
- Viwango vya juu vya kingamwili baada ya chanjo ya nyongeza ambavyo vinaweza kutoa ulinzi zaidi dhidi ya aina mpya za virusi.

Information in this infographic is correct as of February 2022.

Chanjo za UVIKO-19 ni salama na zinatafaa sana katika kuzuia magonjwa makali na vifo.

Hata kama umekuwa na UVIKO-19, chanjo Itaongeza kinga yoyote uliyo nayo kutokana na maambukizi ya awali.

